UPANUZI WA KIWANJA CHA NDEGE MWANZA UTAKAVYONUFAISHA WANANCHI KIUCHUMI

*Zaidi ya wakazi miloni 15 wa Kanda ya Ziwa kusafirisha mboga, maua, nyama nje

*Pinda asema hata wale wa Nchi za Maziwa Makuu watapata fursa za kiuchumi

*TAA yajipanga kuufanya wa kimataifa kama JNIA, KIA zitue ndege Boeing 747

*Safari za wanaotaka kwenda Ulaya, Marekani na Asia sasa kuanzia Mwanza

Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ni moja kati ya viwanja 58 ambavyo vinasimamiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA). Hivi sasa kinafanyiwa upanuzi mkubwa utakaokipandisha hadhi kuwa daraja 4D ambapo ndege za mizigo na abiria za ukubwa wa kiwango cha Boeing 747 na jamii yake, zinaweza kutua na kuruka uwanjani hapo.

Kiwanja hicho ni cha tatu kwa ukubwa wa mindombinu ya kuhudumia ndege, abiria na mizigo na kibiashara baada ya kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) na kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), Jijini Dar es Salaam.

Kiwanja cha ndege cha Mwanza ni kitovu kikubwa cha safari za ndege katika kanda ya Maziwa Makuu na kinaunganisha miji ya nchi jirani na miji yetu kama vile Nairobi, Kisumu (Kenya), Entebbe (Uganda), Kigali (Rwanda), Bukoba, Musoma, na Kigoma.

Kwa kutambua umuhimu wa kiwanja hicho, Serikali ilijiwekea dhamira ya kuboresha miundombinu ya kiwanja hiki kwa kuipanua na kuweka vifaa na mitambo ya kisasa. Katika kutekeleza dhamira hiyo, mwaka 2006 Serikali ilitafuta mkopo wa dola milioni 12 (sh. Bilioni 20) kutoka Benki ya BADEA na Shirika la OFID na yenyewe ikatoa sh. Bilioni 85.

Ziara ya Waziri Mkuu, Pinda Mwanza

Hivi karibuni, Waziri Mkuu, Mh. Mizengo Pinda na ujumbe wake, walitembelea kiwanja hicho ili kujionea maendeleo ya upanuzi mkubwa na ukarabati unaoendelea kufanywa na TAA kwa fedha za Serikali na wahisani kwenye kiwanja hicho ili kiwe cha Kimataifa kama Kiwanja cha Julius Nyerere (JNIA), Jijini Dar es Salaam na cha Kilimanjaro (KIA)

Waziri Mkuu, Mh. Mizengo Pinda aliyekwenda kiwanjani hapo kujionea maendeleo ya kazi ya upanuzi huo Agosti 23 anasema, kiwanja hicho kitasaidia kukuza maendeleo ya kisekta ya wakazi zaidi ya milioni 15 wa mikoa ya Kanda ya Ziwa ambao ni takribani theluthi moja ya Watanzania milioni 45 na hivyo umuhimu wake kwa Taifa ni mkubwa.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Pinda, kiwanja hicho kitasaidia kuharakisha kukua kwa uchumi wa wananchi, makampuni, mashirika na taasisi zilizoko maeneo ya mikoa ya Kanda ya Ziwa na nchi jirani za Maziwa Makuu, Uganda, Rwanda, Burundi, Congo DRC.

Kiongozi huyo anasema, kukamilika kwa upanuzi na ukarabati mkubwa wa kiwanja hicho kutachochea uwekezaji katika kilimo cha mboga mboga, maua, uvunaji wa nyama, samaki ambavyo vinahitajika sana Ulaya na nchi nyingine za Asia na Afrika.

Waziri Mkuu anasema, kiwanja hicho kitasaidiana na kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kusafirisha maua na bidhaa nyingine zinazohitaji ubaridi katika uhifadhi na hivyo kutoa fursa zaidi za kiuchumi kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa na Maziwa Makuu. Kwa sasa samaki husafirishwa hadi Nairobi, Kenya kwa magari yenye vifaa ya kuhifadhi baridi ndipo wasafirishwe hadi Ulaya kwenye soko la kimataifa.

Historia ya kiwanja cha ndege cha Mwanza

Historia ya kiwanja hiki cha ndege cha Mwanza inarudi miaka ya 60 wakati aliyekuwa mmiliki wa mgodi wa almasi Mwadui, Bw. Williamson alipokijenga na kukiendesha ili kurahisisha safari zake za kibiashara kati ya Mwanza, Nairobi, Kenya na Afrika Kusini.

Wakati Tanganyika ilipopata Uhuru Desemba 9, 1961, kiwanja hicho kilichukuliwa na Serikali na huo ndio ukawa mwanzo wa safari ndefu ya maendeleo ya matumizi ya kiwanja hicho hadi kinapofanyiwa upanuzi na ukarabati mkubwa kukipandisha hadhi.

Umuhimu wa kiwanja hicho haukuoenakana wakati wa tajiri wa mgodi wa almasi Mwadui tu bali hata sasa ambapo Serikali imeamua kuwekeza zaidi ya sh. Bilioni 105 kukifanya kiwanja hicho kuwa kitovu cha safari za anga kwa nchi za Maziwa makuu.

Serikali imewekeza fedha hizo ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya chama tawala, CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ambayo mgombea wa CCM, Rais Jakaya Kikwete aliwaahidi wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, kuwa kiwanja hicho kitapanuliwa.

Hata hivyo, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhandisi Dk. Crarles Tizeba anasema mradi huo uko nyuma kwa utekelezaji kwani ulikuwa umalizike mwishoni mwa mwaka huu lakini kutokana na ukosefu wa fedha, sasa umepangwa kumalizika Oktoba 2015 ambao unaangukia kwenye mwaka mwingine wa uchaguzi na hivyo kuibua changamoto kwao.

Alichosema Waziri Tizeba kuhusu kiwanja

Waziri Dk. Tizeba alimweleza Waziri Mkuu, Mizengo Pinda katika taarifa yake kuhusu mradi huo kuwa, kusuasiua kwa mradi huo kutokana na ukosefu wa fedha ni changamoto kwa Serikali na CCM kwa vile mradi huo ni ahadi ya Rais kwa wananchi.

Anasema, hadi sasa, mkandarasi anayefanya ukarabati na upanuzi huo, Kampuni ya Beijing Construction and Engineering Group (BCEG) ya China amelipwa sh. Bilioni 1.6 tu kati ya sh. Bilioni 12 anazodai katika kazi za awali alizokwishakamilisha hadi sasa.

Waziri Dk. Tizeba anasema kazi ya upanuzi pia imechelewa kutokana na kuchelewa kwa malipo ya awali(advance payment kwa mkandarasi), kuchelewa kwa malipo ya madai ya mkandarasi ambapo kati ya sh. Bilioni 8 anazodai, amekwishalipwa sh. Bilioni 1.6.

Waziri anaitaja sababu nyingine iliyocheleweshe kuwa ni usanifu mpya wa jengo la abiria ambalo litaongeza uwezo wa kuhudumia abiria milioni 2 kwa mwaka kutoka abiria 500 wa sasa kwa mwaka wanaohudumiwa na jengo lililopo. Usanifu wa jengo la awali ulilenga kuongeza

abiria hadi milioni moja. Jengo jipya litakuwa na ukubwa wa mita 2,000 sawa na la kiwanja cha Julius cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA).

Ukarabati/upanuzi unaofanyika ni upi?

Kazi zilizopangwa kufanyika ni urefushaji wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita 500 zaidi (kutoka 3,100 za sasa) kwa kiwango cha lami; upanuzi wa maegesho ya ndege za abiria (apron); ujenzi wa jengo jipya la abiria pamoja na miundombinu yake, barabara ya kuingia na kutoka na maegesho ya magari na ujenzi wa kituo cha umeme.

Nyingine ni ujenzi wa jengo la mizigo na barabara ya kuingia na kutoka na maegesho ya magari, maegesho ya ndege (za mizigo) Boeing 747 na jamii yake na barabara za kiungio; ujenzi wa jengo la kuongozea ndege na barabara ya kuingia na kutoka ndege (taxiways) na maegesho ya magari na ujenzi wa mifumo ya maji ya mvua na mfumo wa maji safi na taka kwa ajili ya kiwanja kizima kwani kuna wakati yanafurika kutokana na mto Kimilabagalu kufurika. Urefushaji barabara umehamisha mto usimwage maji hapo.

Waziri anasema, kuwa kuna hatari ya kazi ya ujenzi kusimama kama Serikali na Benki ya BADEA na Shirika la OFID wanaogharamia mradi huo, hawatatoa fedha kwa muda muafaka ili kumlipa mkandarasi huyo hivyo akaomba Serikali ifanye jitihada kuzipata.

Waziri Dk. Tizeba ambaye pia ni mbunge Buchosa wilayani Sengerema mkoani Mwanza, alimwomba Waziri Mkuu kwa msisitizo akisema Serikali iangalie kwa makini suala hilo ikijua kuwa kilio cha wananchi wengi wa kanda ya Ziwa ni jengo kubwa na jipya la abiria (TB) kwani ndilo ambalo wabunge wa kanda hiyo walilipigia kelele hata Bungeni.

Katika kupigia debe fedha za mradi huo, Waziri Dk. Tizeba hakuwa peke yake bali hicho kilikuwa pia ndio kilicho kikubwa pia cha mamlaka husika, TAA inayosimamia mradi huo.

Katika taarifa yake ya maendeleo ya mradi huo kwa Waziri Mkuu, Mkurugenzi wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa (DRA), Mhandisi Thomas Haule naye alimwomba Mh. Waziri Mkuu, Pinda afikishe kilio chao cha kupewa fedha na Serikali kwa kutenga bajeti ya kutosha na kulipa madai

ya mkandarasi kwa wakati mradi huo usikwame kwani ametoa tahadhari baada ya mwezi mmoja, huenda atasimama kazi kabisa.

Maelezo ya Mkurugenzi wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa

Mhandisi Haule alimweleza Waziri Mkuu, Pinda kwa nini TAA inataka mradi huo ukamilike haraka akisema ukiwa tayari, utaongeza idadi ya ndege na abiria maradufu kwa ndege kubwa kutua na TAA itakinadi katika maonesho ya utalii na usafiri wa anga.

Kwa sasa, mashirika ya ndege za abiria na mizigo, kubwa na ndogo za kukodi ambayo hufanya safari zake katika uwanja huo kwa saa 24 ni Fast Jet, Precision Air, Auric Air, Air Tanzania Company Limited (ATCL), Coastal Travellers, Tanzanair. Ya ndege za mizigo ni Astra Aviation, Khalid Air na Safari Express. Yako mengine yatakuja baadaye.

Kwa tafisri ya haraka haraka, alichokuwa anakimaanisha Mhandisi Haule ni Serikali kuona ukweli kuwa, ikitoa fedha za kutosha na kiwanja kikakamilishwa ndani ya muda, kitaanza kuingiza fedha mara moja kwani abiria na mizigo zaidi vitaongezeka kutokana na ndege kubwa za Boeing 747 kuweza kutua na kuruka kutoka kiwanjani hapo.

Lakini zaidi ni ukweli kuwa, TAA itakinadi kiwanja hicho kwenye maonesho ya kitalii na usafiri wa anga duniani, kwa watumiaji, mashirika ya ndege makubwa ya nje ili yalete ndege zao hapo kuchukua abiria na mizigo na kuiingizia TAA na Serikali, mapato zaidi.

Je, fedha za kumalizia kazi hiyo zitapatikana ili wananchi wa Kanda ya Ziwa wafurahi? Katika kujibu swali hilo, Waziri Mkuu, Mizengo Pinda alikiri kwamba, uhaba wa fedha za kukamilisha mradi huo ndani ya muda ni changamoto si kwa TAA tu bali hata Serikali.

Pamoja na kusema kuwa ni changamoto ambayo anaibeba kuitafutia ufumbuzi Hazina, bado aliiomba TAA kuangalia njia mbadala ya kuhakikisha mradi huo haukwami na akaenda mbali zaidi kumwomba mkandarasi, BCEG, kutosimamisha kazi bali aendelee wakati akisubiri malipo yake kwani China ina uhusiano mzuri na Serikali ya Tanzania.

Alimweleza mmoja wa wakandarasi Mchina wakati akikagua jengo jipya la kuongozea ndege, kwamba atazungumza na Balozi wa China nchini Tanzania ili kuangalia namna gani wanaweza kufanya kazi hiyo iendelee bila kusimama wakati fedha zikitafutwa.

Ni wazi, kauli ya Waziri Mkuu, Mizengo Pinda ilikuwa ni ahueni kubwa kwa wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa ambao walishaanza kuingiwa hofu ya kudhani mradi huo hautakamilika kabla ya uchaguzi mkuu wa mwakani, 2015 kama Rais alivyowaahidi.

Changamoto inayochelewesha mradi

Pamoja na ahadi ya Waziri Mkuu, Pinda ya kutafuta fedha Hazina na pia kuitaka TAA kuangalia jinsi gani inaweza kuwasiliana na taasisi binafsi za kuwekeza katika mradi huo, tayari Wizara ya Uchukuzi inayoongozwa na Dk. Harrison Mwakyembe ilishaanza kuangalia njia mbadala ya kuhakikisha kwamba mradi huo haukwami kamwe.

Kwa mujibu wa Waziri Tizeba, kwa mwaka huu wa fedha, 2014/15, Serikali imetenga bajeti ya sh. Bilioni 12 ambayo anasema, ni vyema ikalipwa yote kwa mkandarasi ili mradi usikwame na kusababisha adhabu ya kutozwa faini kwa kucheleweshe malipo.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhandisi Dk. Tizeba pia alimweleza Waziri Mkuu, Pinda katika taarifa yake kwa Kiongozi huyo mkuuu kuwa, Wizara inaangalia uwezekano wa kunyofoa sehemu ya kazi kwenye mradi huo (package) ya ujenzi wa jengo la abiria (TB) ijitegemee na kuitafutia fedha ijengwe peke yake na mkanadarasi mwingine (sio BCEG).

Hata hivyo, Waziri alisema, itabidi wawasiliane kwanza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kuona sheria ya manunuzi inasemaje kuondoa migongano ya kisheria ingawa wanadhani ili kuondoa mgogoro na mkandarasi na pia kucheleweshe mradi kwa kutangaza zabuni mpya, fedha ikipatikana, mkandarasi wa sasa aendelee na kazi hiyo.

Naibu Waziri huyo alisema, TAA ingependa kuona eneo la kipande cha barabara ya kutua na kuruka ndege kinachoongezwa, kinapanuliwa zaidi eneo lake la kudhibiti maji lakini tatizo ni mawasiliano na makamanda wa Kikosi cha Anga cha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ambao eneo hilo linaingia kwenye eneo la jeshi hilo.

Katika kuonesha utayari wa TAA kutekeleza mradi huo bila kutetereka, Waziri Tizeba alimweleza Waziri Mkuu, Mizengo Pinda jinsi taasisi hii ilivyodhamiria kuendelea na upanuzi huo wa kiwanja kwa kukopa fedha kutoka Benki ya Maendeleo (TIB).

TAA yajipanga kujenga kutumia Benki ya TIB

Alisema TAA wana mpango wa kujenga jengo la abiria kwa kupitia uwekezaji wa ubia (PPP) na TIB na kwamba mazungumzo ya awali kati yao yanaendelea vizuri. Pia alisema, kuna wawekezaji wa kutoka nje wameonesha nia ya kuikopesha Serikali kwa ajili ya kukamilisha mradi huo. Waziri Mkuu aliunga mkono wazo hilo la TAA na TIB.

Kauli hiyo ilisisitizwa pia na Mkurugenzi wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa (DRA), Mhandisi Haule. Jambo hilo linaonesha jinsi TAA inavyotekeleza kwa vitendo,dira yake ya kuwa mtoaji huduma za viwanja vya ndege kwa kiwango cha kimataifa.

Pia linaonesha jinsi TAA inavyoendelea kutekeleza kwa weledi, dhima yake ya kutoa hduuma bora na viwezeshi katika viwanja vyake vya ndege kwa kuzingatia ufanisi katika matumizi ya raslimali imani yake kuu ya kuwajali wateja, kufanya kazi kwa pamoja na ulinzi na usalama viwanjani kwa maslahi na maendeleo makubwa ya nchi.

Awali, Mhandisi Haule aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu, Mhandisi Suleiman Said alimweleza Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, historia fupi ya mradi huo tangu kusainiwa mkataba wa kazi Juni 11, 2012, mkandaras, BCEG kuanza kazi Julai 2, 2012. Mhandisi mshauri wa mradi ni Kampuni ya UNETEC ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) anayefanya kazi hiyo kwa gharama za dola 3,376,031 mbali ya zile za mkandarasi.

Kazi alizokwishafanya mkandarasi BCEG

Mhandisi Haule pia alieleza kazi ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu iliyofanyika, iliyokamilika na iliyobaki na mkandarasi anafanya nini kwa sasa na matarajio yaliyopo. Alisema, mkandarasi ameshakamilisha ofisi yake na kukata, kuchimba na kuondoa udongo katika eneo la kurefusha barabara ya kutua na kuruka ndege kwa asilimia 100.

Mkandarasi ameshachimba na kusawazisha udongo eneo la mita 500 za barabara ya ndege na ujenzi wa mitalo ya kutoa maji ya mvua kwenye barabara hiyo (runway) na ameshachimba na kuondoa udongo eneo la usalama wa ndege katika barabara (RESA) kwa mita 240 na ameshajenga tabaka la mawe kina cha mm 500 katika barabara hiyo.

Kwa mujibu wa ratiba ndogo ya ziara iliyotolewa na Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, Esther Madale, Waziri Mkuu alitembelea ujenzi wa mnara mpya wa kuongozea ndege unaojengwa katika moja ya vilima vilivyopo kando ya kiwanja hicho ambapo mkandarasi ameshakamilisha umwagaji zege kutoka msingi hadi ghorofa ya kwanza.

Mkurugenzi wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa (DRA), Mhandisi Haule alimweleza waziri Mkuu, Pinda mkandarasi sasa anafanya matayarisha ya jamvi la ghorofa ya pili na la paa na amekamilisha ujenzi wa nguzo za msingi wa jengo na anaendelea kukata na kuondoa udongo eneo litakalojengwa maegesgo ya ndege za mizigo (apron) na viungio.

Pia alisema mkandarasi anapanua barabara ya kutua na kurukia ndege kutoka mita 3100 hadi 3700 na amekamilisha ujenzi wa kalavati kubwa la urefu wa mita 156 na upana wa mita 8 kutoa maji ya mvua katika barabara ya kutua na kuruka ndege kwa asilimia 100 na usimikaji wa mtambo wa lami na kokoto za kujengea barabara hiyo.

Waziri Mkuu, Pinda pia alielezwa lilipo eneo ambalo jengo jipya la abiria ambalo ukubwa wake utakuwa karibu sawa na jengo la sasa la kiwanja cha Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam mita 2,000 za mraba litakalohudumia abiria milioni 2 kwa mwaka, litajengwa.

Maagizo ya Waziri Mkuu, Pinda kwa uongozi wa TAA, mkoa

Kabla ya kukagua maeneo ya mradi, Waziri Mkuu alizungumza na uongozi wa mkoa wa Mwanza, TAA, wafanyakazi wa mamlaka hiyo na wale wa mkandarasi, BCEG ambapo aliutaka uongozi wa mkoa wa Mwanza kujipanga ili uweze kukitumia vyema kiwanja hicho kitakapokamilika kwa kupanua barabara ya kutoka mjini kwenda Kiwanja cha Ndege na kujenga miundombinu ya sehemu za kuhifadhia bidhaa zinazohitaji ubaridi.

Aliutaka uongozi wa TAA kujipanga zaidi ili kukamilisha kiwanja hicho kwa kulenga soko la theluthi moja ya Watanzania milioni 45 ambao ni wakazi wa Kanda ya Ziwa na kunufaika na soko la kimataifa kwa kufungua kiwanja kitumiwe na ndege kubwa zaidi kwenda nchi za nje katika Ukanda wa Maziwa Makuu, Kigali, Rwanda, Bujumbura, Burundi, DRC, Nairobi, Kenya na maeneo mengine na kurahisisha usafiri na biashara.

Aliutaka pia uongozi wa mkoa wa Mwanza kuwaandaa wananchi kwa biashara za mazao ya kilimo kama mboga mboga, maua, samaki, nyama zinazohitaji kusafirishwa masoko ya nje na sasa zinapelekwa kupitia kiwanja cha kimataifa cha Kilimanjaro (KIA).

Waziri Mkuu, Pinda pia aliutaka uongozi wa TAA kwa kushirikiana na Jiji na Manispaa ya Ilemela kiliko kiwanja, kuhakikisha wanayalinda maeneo ya kiwanja hicho yasivamiwe na wananchi kujenga makazi na hivyo kuja kulazimika kulipa fidia baadaye kama ilivyofanyika Kipunguni na Kigilagila kwa upanuzi wa kiwanja cha Julius Nyerere (JNIA).

Aliutaka uongozi wa Jiji kuangalia jinsi gani ya kuimarisha barabara inayozunguka kiwanja cha ndege na kutokea Kisesa ili kuiimarisha na kuifanya iwe kiungo kati ya kiwanja hicho na Hifadhi ya Serengeti na hivyo kukifanya kiwanja Gateway to Serengeti.

Pia aliupa changamoto uongozi wa Jiji kuangalia jinsi ya kushirikiana na sekta binafsi kupitia PPP kuimarisha na kukuza kiwango cha maonesho ya 77 karibu na kiwanja hicho yawe na sura ya kimataifa na yafanyike mwaka mzima kukipa msukumo wa kibiashara.

Pinda atembelea eneo la mradi kuona kazi iliyofanyika

Waziri Mkuu, Pinda alipotembelea mnara wa kuongozea ndege alisisitiza umuhimu wa kutunza maeneo yanayozunguka kiwanja yasiporwe na kuitaka TAA kuongeza njia ya pili ya kutua na kurukia ndege ili kuongeza miruko ya ndege na idadi ya ndege hapo.

Akiwa kwenye jengo la mnara wa kuongozea ndege juu kilimani, Waziri Mkuu, Pinda alielezwa umejengwa huko ili waongoza ndege waweze kuuona uwanja wote hata kwa macho kulingana na sheria za usalama wa anga zinazotaka mwongoza ndege auone uwanja wote kwa macho na vifaa vya kuongozea ili vifaa vikishindwa, ajue cha kufanya.

PM alifurahishwa na mnara na huo na kushauri kujengwe mawe ya kuzuia mmonyoko. Baada ya kutoka kwenye mnara, alitembelea mtambo wa kuchakata lami na kokoko na kuelezwa na Mhandisi mshauri, Geoffrey Asulemenye jinsi mtambo huo unavyofanya kazi kwa kuchekecha vumbi na kulifanya lisisambae na kuathiri afya za wakazi wa jirani.

Aliutaka uongozi wa Manispaa ya Ilemela na Jiji la Mwanza kuangalia jinsi ya kutumia mtambo huo wa lami baada ya mkandarasi kumaliza kazi yake mwakani, Oktoba 2015. Akiwa barabara ya kurukia ndege na kutua, alifurahia umahiri wa kuweka tabaka kubwa la zaidi ya mita tatu za ujazo kujenga mita 700 zilizoongezwa urefu uliodhihirisha ilivyo gharama kubwa kujenga njia za kuruka na kutua ndege tofauti na barabara za magari.

Alishauri eneo la ardhi ya kiwanja liwekwe uzio na alama za watu kutojenga ili kulilinda na TAA waongeze ardhi zaidi kwa maendeleo ya baadaye ya upanuzi wa uwanja huo.

Ziara ya Waziri Mkuu, Pinda ilikuwa sehemu ya ziara ya Kiserikali aliyoifanya katika mkoa wa Mwanza kukagua miradi miradi ya maendeleo na kuendesha harambee ya Mfuko wa Benjamin Mkapa ambapo pia alitembelea pia mradi wa jengo la kitega uchumi la Machinga Complex linalojengwa na Mfuko wa LAPF, moja ya vitega uchumi vinavyolifanya Jiji la Mwanza liende na wakati hasa wakati huu uwanja unapopanuliwa.

Matumaini ya wakazi wa Mwanza kuhusu kiwanja kukamilika

Je, maagizo yake yatatekelezwa? Swali hilo linajibiwa na hali halisi ya maendeleo ya mradi huo aliyoyaona ambayo, ukiacha tatizo la fedha, yanatia matumaini makubwa ya mradi huu kuwa mkombozi mkubwa wa maendeleo ya wakazi wa Kanda ya Ziwa.

Uwepo kwenye ziara hiyo, kwa Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Mwanza, Dk. Athony Diallo, Mkuu wa mkoa wa Mwanza, Mhandisi Evarist Ndikilo, Mkuu wa wilaya ya Ilemela, Amina Masenza, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela na wakuu wa vyombo vya usalama kunatosha kuashiria kuwa, mradi huo utasimamiwa ipasavyo uishe.

Kukamilika kwa upanuzi na ukarabati wa kiwanja cha Mwanza siyo tu utawezesha ndege kubwa zaidi kufanya safari za kimataifa za masafa marefu (intercontinental) kwenda Ulaya, Asia na

kwingineko kutokea Mwanza na siyo Kilimanjaro (KIA) na Dar es Salaam (JNIA) tu, bali kutaonesha jinsi TAA inavyounga mkono maendeleo ya kitaifa na kiuchumi kwa kuhakikisha kunakuwepo miundombinu na huduma muhimu viwanjani.

Pia kutaonesha jinsi TAA inavyoendesha, kusimamia, kutunza na kuendeleza viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali Tanzania bara na kufikia malengo ya kuongeza mbinu za upatikanaji wa mapato kwa kuvutia vitega uchumi vya ziada katika viwanja vya ndege inavyovisimamia ili kupata ziada ya mapato ya kutekeleza mikakati yake.

Mwandishi wa Makala haya, Godfrey Lutego ni Afisa Uhusiano wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) simu 0713507777